**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI (R) (MST.) SEMISTOCLES S. KAIJAGE KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO CHA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI NA WAWAKILISHI WA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA MWL. J. K. NYERERE**

**TAREHE 18 AGOSTI, 2020**

- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume,**
- **Mkurugenzi wa Uchaguzi,**
- **Waheshimiwa Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu,**
- **Watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,**
- **Wanahabari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

*Bwana Asifiwe,*
*Tumsifu Yesu Kristo,*
*Assalam Aleykum.*

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na kutuwezesha kukutana siku ya leo kwa ajili ya kikao hiki muhimu. Umuhimu wa kikao hiki unatokana na jukumu kubwa la maandalizi ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2020 ambapo sisi tuliopo hapa ni wadau wake muhimu. Aidha, niwashukuru kwa kuitikia wito wetu wa kuhudhuria kikao hiki lakini pia kwa uvumilivu wenu kwa kuwa mara kadhaa mmeonesha nia ya kuonana na viongozi wa Tume, lakini ikawa ni vigumu kutokana na ratiba na majukumu mengine ya Tume, kwa mujibu wa mpango kazi kueleka siku ya uchaguzi.

Hata hivyo, Tume ilishapanga muda muafaka wa kukutana nanyi ambao ni siku ya leo. Pamoja na kwamba lengo la kukutana nanyi leo ni kutoa taarifa ya maandalizi na maelekezo mbalimbali kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Tume itatumia fursa hii pia kusikiliza hoja zenu na changamoto mbambali zinazowakabili na kuona namna ambavyo inaweza kuzitatua zile ambazo ziko ndani ya uwezo wake.

Aidha, kikao hiki pia kinalenga kutimiza ahadi yetu ambayo tumekuwa tukiitoa kwenu mara kwa mara ya kuwashirikisha katika hatua mbalimbali za michakato ya uchaguzi kwa kadri inavyowezekana. **Karibuni sana**.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, Tume imekamilisha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambao ulifanyika mara mbili kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 15 (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 21 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Uboreshaji wa Daftari ulianza tarehe 18 Julai, 2019 na kukamilika 20 Juni, 2020. Katika kipindi hicho, awamu mbili za uboreshaji wa daftari zilifanyika halikadhalika uwekaji wazi wa daftari la awali.

Katika awamu zote mbili, uboreshaji ulifanyika katika vituo **37,814** vya kuandikisha wapiga kura**. K**atika zoezi hilo Jumla ya Wapiga Kura wapya **7,326,552** waliandikishwa sawa na asilimia **31.63** ya Wapiga Kura **23,161,440** walioandikishwa mwaka 2015. Aidha, Jumla ya

Wapiga Kura **3,548,846** waliboresha taarifa zao na Wapiga Kura **30,487** waliondolewa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutokana na kukosa sifa kwa mujibu wa sheria. Baada ya kuwaondoa Wapiga Kura ambao taarifa zao zimejirudia, kwa hivi sasa Daftari lina jumla ya Wapiga Kura wapatao **29,188,347.**

Kutokana na idadi hiyo ya wapiga kura, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kutakuwa na vituo **80,155** vya kupigia kura na kila kituo kimoja kitakuwa na Wapiga Kura wasiozidi **500**.

Kama mtakumbuka katika zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Tume iliahidi kukusanya taarifa za watu wenye ulemavu. Baada ya mchakato wa kuchambua taarifa za wapiga kura kwenye Daftari imebainika kuwa kati ya Wapiga Kura wapya **7,326,552** walioandikishwa katika awamu zote mbili za uboreshaji, wapiga kura **13,211** ni watu wenye ulemavu. Kati yao, wapiga kura **2,223** wana ulemavu wa macho, wapiga kura **4,911** wana ulemavu wa mikono na wapiga kura **6,077** wana ulemavu wa aina nyinginezo.

Takwimu hizi zinahusu wapiga kura walijitokeza katika kipindi cha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wa mwaka 2019/2020 na hazihusishi wapiga kura walioandikishwa mwaka 2015. Hata hivyo, Takwimu hizi zitaisadia Tume na ninyi wa wakilishi wa watu wenye ulemavu, katika kujipanga kwa lengo la kuliwezeshsha kundi hili kutimiza haki yao ya msingi ya kikatiba ya kuchagua viongozi wanaowataka, kwa kadri itakavyowezekana.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Katika kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, hakukuwa na marekebisho katika Sheria za Uchaguzi. Isipokuwa, Tume imefanya maboresho ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020. Vile vile, imekamilisha Maelekezo ya Uchaguzi kwa ajili ya Watendaji wa Uchaguzi na wadau mbalimbali.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Ili kuwa na uwazi katika zoezi la Uchaguzi Mkuu, Tume imekuwa ikiwashirikisha wadau wa uchaguzi, mkiwemo ninyi watu wenye ulemavu, katika hatua mbalimbali za mchakato wa Uchaguzi. Mathalan, mtakumbuka kuwa kabla ya kuanza zoezi la uboreshaji, Tume ilikutana na wadau mbalimbali mkiwemo ninyi na kupokea maoni yenu.

Maeneo mengine ya ushirikishwaji wa wadau yalihusu nyaraka zinazohusu zoezi la uboreshaji ambapo Tume iliwapatia wadau nyaraka mbalimbali kama vile orodha ya vituo vya uandikishaji vya nchi nzima, Kanuni za Uboreshaji na ratiba za mazoezi mbalimbali. Katika uchaguzi mkuu huu, Tume itavipatia vyama vya siasa orodha ya vituo vya kupigia kura kwa lengo la kuvitambua vituo hivyo nchi nzima. orodha hiyo pia itavisaidia vyama vya siasa katika kupanga mawakala wa kila kituo cha kupigia kura.

Wadau wengine ambao Tume imekuwa ikiwashirikisha ni Vyombo vya Habari, Makundi Maalum katika jamii kama vile Wanawake, Vijana, Asasi za Kiraia na katika baadhi ya maeneo, Wazee wa Kimila.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Kama ambavyo imeripotiwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilikwisha tangaza ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kama ambavyo mmesikia, Uchaguzi Mkuu umepangwa kufanyika siku ya Jumatano tarehe 28 Oktoba, 2020.

Serikali kwa upande wake tayari imetoa tamko la kuitangaza siku hiyo kuwa ni siku ya mapumziko.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Fomu za Uteuzi zilianza kutolewa tarehe 5 Agosti, 2020 kwenye Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jijini Dodoma kwa wagombea wa Kiti cha Rais. Hadi sasa vyama vya siasa 16, tayari vimechukua fomu hizo. Aidha, Fomu kwa ajili ya wagombea Ubunge na Udiwani zimeanza kutolewa tarehe 12 hadi 25 Agosti, 2020 kwenye Makao Makuu ya Halmashauri yalipo Majimbo na Kata husika.

Aidha, urejeshaji wa fomu utafanyika tarehe 25 Agosti, 2020 kabla ya saa 10 kamili jioni, ambayo ndiyo siku ya uteuzi.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi, kampeni zitaanza tarehe 26 Agosti hadi tarehe 27 Oktoba, 2020. Katika kipindi cha kampeni, vyama vya siasa vitapata fursa ya kuwanadi wagombea wao na kuelezea sera na Ilani za Uchaguzi za vyama vyao.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Katika maandalizi ya uchaguzi mkuu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilishirikiana na Vyama vya Siasa pamoja na Serikali katika kuandaa Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 ambayo yalisainiwa na pande zote mnamo tarehe 27 Mei, 2020.
Maadili haya, yanasimamia michakato ya uchaguzi ikiwa ni pamoja na mienendo ya Kampeni za Uchaguzi na yameweka makatazo mbalimbali, kwa kubainisha mambo yanayotakiwa na yasiyotakiwa kufanywa na wahusika.

Maadili ya Uchaguzi, pamoja na mambo mengine, yanavitaka Vyama vya Siasa kufanya Kampeni za kistaarabu na kuepuka kufanya fujo au kuchochea vurugu za aina yoyote katika mikutano ya vyama vingine; kutokutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, ulemavu, rangi au maumbile kwenye mikutano na kwenye shughuli zote za kampeni na kadhalika.

Jambo linalotia moyo ni kwamba kamati za maadili katika ngazi zote, wajumbe wake ndiyo wahusika wa maadili ya uchaguzi ambao ni Tume, Serikali na Vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi katika ngazi husika. Kwa mantiki hiyo, suluhu ya migogoro yote ya kimaadili itapatikana kwa wahusika wenyewe kupitia kamati zitakazoundwa.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu**;

Napenda kutumia nafasi hii pia kuwapa taarifa kuhusu maeneo mengine muhimu katika kufanikisha Uchaguzi Mkuu, ambayo ni bajeti na vifaa vya uchaguzi. Katika kuandaa na kuendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, Tume iliandaa Bajeti ya kiasi cha **Tsh. 331,728,258,035.00** zinazotarajiwa kutumika. Kwa kuzingatia kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina, itagharimia shughuli zote za Uchaguzi kwa asilimia mia moja.

Katika eneo la vifaa vya uchaguzi Tume inaendelea na mchakato wa ununuzi wa vifaa mbalimbali sambamba na uchapishaji wa fomu, sheria za uchaguzi, kanuni na maelekezo. Jumla ya zabuni ishirini na tano (25) zimetangazwa ambazo zinahusisha uchapishaji wa nyaraka au ununuzi wa vifaa mbalimbali vya uchaguzi,

Elimu ya Mpiga Kura ni eneo lingine muhimu katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu. Kwa mujibu kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 Tume imepewa mamlaka ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia Taasisi au Asasi zenye nia ya kutoa elimu hiyo.

Hivyo, Tume kwa upande wake imejipanga kutoa elimu hiyo kwa njia mbalimbali zinazojumuisha Vyombo vya Habari, Mitandao ya Kijamii, Machapisho mbalimbali, Mikutano na wadau, kushiriki katika maonesho na matamasha mbalimbali kwa mfano hivi karibuni Tume imeshiriki katika maonesho ya wakulima 88 katika mikoa ya Morogoro na Dodoma na kutumia gari la Matangazo la Tume kwa ajili ya kukutana na wananchi ana kwa ana na kwa sasa gari hilo katika mikoa ya kanda ya ziwa kikiendelea na jukumu hilo.

Tume pia imetoa vibali kwa jumla ya asasi 252 zilizokidhi vigezo kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura wakati wa Uchaguzi Mkuu. Kati ya Asasi hizo, saba (7) ni kutoka Tanzania Zanzibar. Na hivi karibuni, Tume inatarajia kukutana na Asasi hizo ili kuwapitisha katika Mwongozo wa kutoa Elimu ya Mpiga Kura wanaopaswa kuutumia na kuufuata katika kipindi chote cha zoezi hili.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Katika ushirikishaji wa wadau, Tume pia iliwaalika Watazamaji wa Uchaguzi wa ndani ambapo jumla ya Asasi 97 zilizokidhi vigezo tayari zimepewa taarifa na zinasubiri kupewa vibali wakati ukifika.

Kwa upande wa Watazamaji wa Uchaguzi wa Kimataifa, mwaliko umetolewa na zoezi la kupokea maombi linaendelea. Mchakato huo utakapokamilika, taarifa rasmi itatolewa.

Kama ilivyokuwa katika uchaguzi wa 2015, Idadi ya majimbo ya uchaguzi imebaki **264**, ambapo Tanzania Bara ina Majimbo **214** na Tanzania Zanzibar ina Majimbo **50**. Idadi ya Kata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu itakuwa ni **3,956**.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Kwa kuwa kupiga kura na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ni haki yenu ya kikatiba, bila shaka mmeshiriki kikamilifu katika mchakato wa kuwapata wagombea ndani ya vyama vya siasa ambao hatimaye watagombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Kwa kadri inavyowezekana Tume itaendelea kuhakikisha kundi la watu wenye ulemavu linashiriki katika michakato hii ya uchaguzi kikamilifu. Njia mojawapo ni kutoa maelekezo kwa watendaji wa uchaguzi kutoa kipaumbele kwa watu wenye mahitaji maalumu hasa siku ya kupiga kura. Pia, Tume itaandaa karatasi za kura zenye maandishi ya nukta nundu ili kuwawezesha wasiiona kupiga kura wenyewe. Wale ambao hawataweza kutumia karatasi za kura zenye nukta nundu wataruhusiwa kwenda vituoni na watu wa kuwasaidia.

Kwa wenzetu wenye ulemavu wa viungo ambao hawawezi kusimama na hivyo kushindwa kutumia vituturi kama vilivyo, Tume imeandaa vituturi ambavyo vikigeuzwa chini-juu vitawawezesha watu wenye ulemavu wa viungo kuweza kuvitumia.

Katika kipindi hiki, Tume itatumia wakalimani wa lugha za alama ili kuwawezesha watu wenye ulemavu wa kusikia kufuatilia na kupata elimu na taarifa mbalimbali zinazotolewa na Tume

katika mikutano mbalimbali. Mazungumzo yanaendelea na vyombo mbalimbali vya habari kuona namna watakavyowatumia wakalimani hao katika matangazo yao.

Aidha, katika kutoa elimu Tume itaendelea kutoa machapisho na matangazo ya runinga ambayo yatagusa makundi yote katika jamii kulingana na mahitaji yao. Mfano mzuri ni machapisho katika mfumo wa picha na matangazo ya runinga katika mfumo wa michezo ya kuigiza ili kuwawezeshaa sio tu watu wenye ulemavu wa kusikia lakini pia wasiojua kusoma na kuandika.

**Ndugu Wawakilishi wa Watu wenye Ulemavu;**

Tume ina matumaini makubwa ya kufanikisha Uchaguzi huu kwa kutegemea ushiriki wenu. Imani hii inatokana na ushirikiano mlioonesha wakati wote tangu wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura. Mmekuwa wepesi wa kuwasilisha hoja na ushauri na kutaka ufafanuzi pale inapohitajika kila tunapokutana nanyi katika vikao mbalimbali.

Baada ya kupokea hoja, ushauri, maoni na mapendekezo yenu katika kikao hiki, Tume itayafanyia kazi na baadaye kutakuwa na kikao cha pamoja kutoa mrejesho wa namna changamoto zilizojitokeza zimeweza kushughulikiwa. Kikao hicho kitakuwa ni kati ya sekretarieti ya Tume na wawakilishi wenu kulingana na mahitaji ya kila kundi husika.

Kwa mara nyingine, napenda kuwashukuru tena kwa kuitikia wito na kushiriki kikao hiki muhimu kwetu sote. Tume itaendelea kuwashirikisha kwa kadri itakavyowezekana, na kama kawaida itasimamia uchaguzi huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali zinazosimamia uendeshaji wa uchaguzi. Lengo likiwa ni kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 unakuwa huru, wa uwazi, wa haki na wa kuaminika kwa kuweka mazingira sawa ya ushindani kwa wagombea wa vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki.

***Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutamka rasmi kuwa kikao chetu kimefunguliwa rasmi.***

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**